

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS  
NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

Geita  
13 Oktoba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema katika kuimarisha manufaa wanayopata Watanzania kupitia sekta ya madini, mwelekeo wa Serikali ni madini hayo kuongezewa thamani hapa nchini, kuwezesha Benki Kuu ya Tanzania kuwa na akiba ya dhahabu, na kuhakikisha kuwa wenye leseni za uchimbaji madini wanazitumia kikamilifu.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo wakati akifunga Maonesho ya Saba ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika katika viwanja vya Kituo cha Uwekezaji cha Bombambili.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema ni hatua muhimu kwa wadau kukutana na kubadilishana uzoefu, teknolojia na kupata elimu ya fursa zinazopatikana kwenye sekta ya madini katika kuimarisha uwekezaji na kuongeza ushiriki na manufaa kwa Watanzania kupitia sekta hii.

Hali kadhalika, Rais Dkt. Samia amesema Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuhakikisha Tanzania inakuwa na akiba ya kutosha ya dhahabu kupitia wamiliki wa leseni na wafanyabiashara wa madini kutenga asilimia 20 ya dhahabu inayozalishwa nchini na kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania.

Awali, Rais Dkt. Samia alitembelea kiwanda cha Geita Gold Refinery na Soko la Madini la Geita ambalo ni moja kati ya masoko 44 katika mikoa yote na vituo 103 vya kununulia madini, na kutoa rai kwa wachimbaji wadogo kuendelea kutumia masoko hayo ambayo yanawahakikishia soko la uhakika.

Vilevile, leo Rais Dkt. Samia amekagua maendeleo ya ujenzi wa Daraja la JP Magufuli linalounganisha eneo la Kigongo (Misungwi) na Busisi (Sengerema) lenye urefu wa kilomita 3, na kusalimiana na Bi. Juliana Stephano Kidaso mama mzazi wa Mama Janeth Magufuli.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu





Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,  
**Jtokeze Kushiriki Uchaguzi**